RAIA MWEMA
JUMATATU, Machi 28, 2022



Waziri wa Fedha na Mipango, Mwigulu Nchemba (kulia) akizungumza jambo kwenye kikao chake na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (kushoto), kujadili namna nyongeza ya bajeti inavyotarajiwa katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kilichofanyika Dodoma juzi. (Picha na [illegible])

# Kilimo, mifugo, uvuvi kuongezwa bajeti

**Na Benny Mwaipaja, Dodoma**

WAZIRI wa Fedha na Mipango Dk Mwigulu Nchemba, ameahidi kuwa Serikali, katika bajeti ya mwaka 2022/23, itaongeza fedha kwenye kilimo, mifugo na uvuvi ili sekta hizo zichangie kipato cha wananchi na Taifa kwa ujumla.

Alitoa ahadi hiyo jijini hapa juzi, alipokutana na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, kujadili uwekezaji wa fedha za umma unaokusudiwa kufanywa kwenye wizara yake unavyoweza kuongeza tija katika sekta ya mifugo na uvuvi.

Alisema sekta ya mifugo na uvuvi ikiwekewa miundombinu ya uhakika inaweza kuleta mapinduzi makubwa ya kipato cha wananchi na kuliwezesha Taifa kukuza uchumi wake.

Dk Mwigulu alitolea mfano wa uendelezaji ranchi za Taifa, kukuza uvuvi kwa kuwekeza kwenye vitendea kazi vya uhakika zikiwamo boti za uvuvi kuwezesha nchi kuzalisha mazao ya mifugo na uvuvi kwa wingi, na kuuza nje ya nchi ili kupata fedha za kigeni.

Alimshauri Waziri Ndaki kuelekeza rasilimali fedha watakazopewa kwenye maeneo ya viwanda vya kuchakata nyama na maziwa, ili kuongeza thamani na kuwezesha upatikanaji wa malighafi kwenye viwanda hivyo.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Lawrence Mafuru alisisitiza kuwa malengo ya kutaka kuipa Wizara hiyo fedha nyingi ni kuonesha kuwa sasa Serikali inataka kuona fedha hizo zinakuwa uwekezaji badala ya matumizi ya kawaida.

Alisema sekta muhimu kama kilimo, mifugo na uvuvi zikiboreshwa, zitaleta matokeo makubwa na chanya kiuchumi na kijamii kwa sababu zitakuza ajira, zitaongeza wigo wa mauzo nje ya nchi na kuondolea wananchi umaskini wa kipato, na hivyo nchi kulipa deni lake.

Ndaki, alieleza kuwa fedha zitakazotolewa na Serikali zitaelekezwa katika kuboresha uvuvi kwani wanatarajia kununua boti 348, kujenga mialo na masoko ya kuuzia samaki kwenye maeneo ya kimkakati.

Katika mifugo, alisema nguvu zaidi zitaelekezwa kwenye maeneo ya kuboresha mifugo kupitia ranchi za Taifa na makundi maalumu ya wafugaji.

Pia kuimarisha huduma za ugani na kunenepesha mifugo, ili iwe na tija, akisema sekta hizo kwa kuanzia, zitahitaji zaidi ya dola za Marekani milioni 105, sawa na takribani Sh bilioni 270.

# Waombwa ushirikiano uandikishaji anuani

**Na Raymond Mihayo, Kahama**

MADIWANI wa Halmashauri ya Manispaa, wametakiwa kutoa ushirikiano katika uandikishaji [illegible] za makazi, ili kuweka historia [illegible] wao kwa mara ya kwanza [illegible] uhuru.

[illegible] kuwa madiwani wa kwanza [illegible] hili tangu nchi ipate uhuru kwa [illegible] tunaomba mtoe ushirikiano kwenye [illegible] kwani kwa kufanya hivyo ni [illegible] kubwa kwa Taifa lenu kufanikisha [illegible]

[illegible] yalisemwa juzi na Mwenyekiti wa [illegible] Cha Mapinduzi (CCM), Thomas Muyonga akitoa salamu za chama hicho katika Baraza Maalumu la Madiwani lililoketi juzi, kujadili uandikishaji wa anwani za makazi unaotarajia kufanyika hivi karibuni.

Alisema wao CCM wanamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kufanikisha hili, kwani moja ya utekelezaji mkubwa wa Ilani ya CCM na kuwataka madiwani, wataalamu na watendaji kuunga mkono.

Aliendelea kusema kuwa kufanikiwa hilo, ni mwanga katika kuelekea Tanzania yenye maendeleo na kuongeza kuwa madiwani katika kipindi hiki wataandika historia ya wao kuwa wa kwanza kuanzisha hili la anwani za makazi nchini.

Aliwataka madiwani kujua kuwa wana kazi kubwa ya kupeleka ujumbe huo hadi ngazi za chini, kwani jambo hili si dogo na linahusika sehemu zote hadi serikali za mitaa ambapo wenyeviti ndio walinzi wa maeneo yote.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa, Clemence Mkusa alisema kazi hiyo inaendelea nchi nzima na ilizinduliwa Februari 8 mwaka huu na itasaidia kutambua wakazi na kazi zao.

Alisema nia ni kujua utambulisho na kutambua wakazi na shughuli wanazofanya na kuwa mfumo huo ulianza kutumika miaka 50 iliyopita na itasaidia mitaa kuwa na majina na nyumba kuwa na namba.

# Wadau bidhaa za ngozi walia na tozo

**Na Gift Mongi, Moshi**

WADAU wa sekta ya ngozi nchini wameiomba Serikali kuona namna ya kupunguza baadhi ya tozo katika bidhaa hiyo ili kurahisisha upatikanaji wake kwa kuwa kwa sasa ambapo ngozi imeadimika.

Wamesema kama si kukithiri vikwazo hivyo, kungesaidia kuanzishwa viwanda vingi vidogo vidogo ambavyo mbali na kuzalisha ajira, pia kungechangia kuimarika kwa soko la ndani la bidhaa za ngozi.

Hajah Mfinanga wa Kileo wilayani Mwanga, ambaye ni muuza ngozi alisema biashara hiyo kwa sasa inakwenda kwa kusuasua na jambo ambalo lisipowekewa umakini wa ziada itakufa.

Alisema kutokana na kukosekana kwa soko la uhakika la ndani kwa kiasi kikubwa, imechangia wafanyabiashara wasio waaminifu kutumia njia za panya na kutorosha ngozi nje ya nchi.

"Hakuna soko la uhakika tozo zimekuwa nyingi sasa wafanyabiashara badala ya kukusanya ngozi na kuuza katika soko la ndani, baadhi wasio waaminifu wamekuwa wakitumia njia za panya na kuiuza nje ya nchi na kusababisha uhaba wa bidhaa hiyo," alisema.

Alisema kutokana na hali ilivyo huenda viwanda vya ndani vinavyozalisha bidhaa za ngozi vikakosa malighafi, kwani ngozi nzuri yote inapelekwa nje ya nchi kimagendo na inayobaki ni kama makapi haifai katika uzalishaji.

Mkurugenzi wa kiwanda cha Woisso Original Products (WOP), Kenneth Woisso alisema hivi karibuni, biashara ya ngozi inapita katika wakati mgumu, kwani ngozi zimeadimika na nyingi zinasafirishwa nje ya nchi.

Alisema ngozi nzuri yote imekuwa ikisafirishwa nje ya nchi na inayosalia ni mbovu, haifai kwa matumizi ya uzalishaji na kuiomba Serikali kuona namna ya kukabiliana na tatizo hilo, lengo likiwa ni kuvinusuru viwanda vya ndani ambavyo pia vinazalisha ajira.

"Sisi wazalishaji wa bidhaa za ngozi kwa siku za karibuni tunapitia kipindi kigumu kwani hakuna malighafi na hata ukipata zipo chini ya kiwango, yaani hazifai katika uzalishaji wa bidhaa," alisema Mkurugenzi huyo.

Alisema katika sekta hiyo ya ngozi kwa sasa zipo changamoto kuu mbili ambayo ni asilimia 10 ya kodi ya huduma kwenye ngozi iliyosindikwa.

Changamoto nyingine ni asilimia 80 ya kodi ya huduma kwenye ngozi ghafi ambapo kiwango hiki kikipungua, huenda biashara hiyo ikawa katika sehemu sahihi zaidi ya ilipo. "Kutokana na kiwango hiki kikubwa cha kodi kumechangia ngozi nyingi kubaki mikononi mwa wafanyabiashara, huku sisi tunaohitaji kama malighafi tukikosa," alisema Woisso.

Alisema kutokana na hali hiyo, sasa ipo haja Serikali kuangalia changamoto hizi kwa undani na kutoa suluhisho, ili kudhibiti baadhi ya wafanyabiashara kuingiza au kuuza ngozi kwa njia ya magendo.

Scanned with CamScanner

RAIA MWEMA
Jumatatu Machi 28, 2022

# Zinahitajika jitihada kuokoa soko la ngozi

**Na Gift Mongi**

KUKOSEKANA kwa usimamizi madhubuti wa kisera na kimfumo kunatajwa kuwa ni miongoni mwa sababu zinazosababisha sekta ya ngozi nchini kuendelea kuzorota siku hadi siku jambo linalotishia uhai wa biashara hiyo.

Wadau wa sekta hiyo wanasema kama sio kushamiri kwa vikwazo hivyo, kungeweza kusaidia kuanzishwa kwa viwanda vingi vidogo vidogo ambavyo mbali na kuzalisha ajira pia vingechangia kuimarika kwa soko la ndani la bidhaa za ngozi.

Takwimu zinaeleza kuwa Tanzania ni nchi ya tatu barani Afrika kwa kuwa na idadi kubwa ya mifugo ikitanguliwa na Afrika Kusini pomoja na Ethiopia.

Kwa mantiki hiyo ni dhahiri uwepo wa idadi kubwa ya mifugo kunaweza kuongeza malighafi yatokanayo na mazao ya mifugo kama nyama, kwato, na hata ngozi ambazo hutumika katika shughuli mbalimbali za kimaendeleo yaani uzalishaji au utengenezaji bidhaa.

Rajab Mtinanga mkazi wa Kileo wilayani Mwanga, Mkoa wa Kilimanjaro ambaye ni muuzaji wa ngozi, anasema biashara hiyo kwa sasa inaenda kwa kusuasua.

Anasema kutokana na kukosekana kwa soko lenye uhakika la ndani kwa klasi kikubwa imechangia wafanyabiashara wasio waaminifu kutumia njia za panya na kutorosha ngozi nje ya nchi.

"Hakuna soko la uhakika na tozo zimekuwa nyingi ambapo wafanyabiashara badala ya kukusanya ngozi na kuiuza katika soko la ndani, baadhi wasio waaminifu wamekuwa wakitumia njia za panya kuiuza nje ya nchi na kusababisha uhaba wa bidhaa ya ngozi," anaeleza Mtinanga.

Pia anasema kuwa kutokana na hali hiyo, huenda viwanda vya ndani vinavyozalisha bidhaa za ngozi vikakosa malighafi, kwani ngozi nzuri yote ndio inayopelekwa nje ya nchi kimagendo na inayobaki ni kama makapi ambayo haifai katika uzalishaji.

Mchuuzi wa ngozi wilayani Hai, Japhet Uronu anasema kwa sasa thamani ya ngozi imeshuka na kwamba wapo wafanyabiashara kutoka nchi jirani wanakuja kununua kwa bei nzuri.

"Sasa kuliko mtu akusanye ngozi halafu bado usafiri na kodi mbalimbali anaona ni bora akusanye tu halafu mnunuzi anakuja kuinunua mara moja na usumbufu kunakuwa hakuna," anaeleza Uronu.

Dalali wa ngozi eneo la Bomang'ombe wilayani Hai, Grace Munisi anasema kuwa kinachochangia kuharibika kwa sekta hiyo ni kukosa dira na mwelekeo, hivyo kila mtu kufanya anavyojisikia ili mradi aweze kutengeneza faida.

"Kwa mfano sasa kufanyike jitihada za kuongeza tozo kwa ngozi ambayo inapelekwa nje hapa ni kuwa tozo ikiwa juu hawatapeleka tena maana kutakuwa hakuna faida na ni njia mojawapo katika kuvinusuru viwanda vya ndani," anasema.

Mkurugenzi wa Kiwanda cha Woisso Original Products (WOP), Keneth Woisso anasema kwa siku za karibuni biashara ya ngozi inapita katika wakati mgumu kwani ngozi zimeadimika na nyingi zinasafirishwa nje ya nchi.

Anasema ngozi nzuri yote imekuwa ikisafirishwa nje ya nchi na inayosalia ni mbovu haifai kwa matumizi ya uzalishaji. Woisso anaiomba Serikali kutafuta mbinu za kutatua changamoto hiyo ili kuvinusuru viwanda vya ndani.

"Sisi wazalishaji wa bidhaa za ngozi kwa siku za karibuni tunapitia kipindi kigumu, hakuna malighafi na hata ukipata unazikuta zipo chini ya kiwango yaani hazifai katika uzalishaji wa bidhaa," anasema Woisso na kuongeza;

"Katika sekta ya ngozi kwa sasa zipo changamoto kuu mbili; ambayo ni asilimia 10 ya kodi ya huduma (export levy) kwenye ngozi iliyosindikwa hadi kufikia wett blue. Nyingine ni asilimia 80 kodi ya huduma (export levy) kwenye ngozi ghafi, ambapo kiwango hiki kikipungua huenda biashara hii ikawa sehemu sahihi zaidi ya hapa ilipo."

Anasema kuwa kutokana na kiwango hicho kikubwa cha kodi kumesababisha ngozi nyingi kubaki mikononi mwa wafanyabiashara huku wahitaji wa malighafi wakizikosa.

Mkurugenzi huyo anaeleza kuwa kutokana na hali hiyo ipo haja kwa Serikali kuangalia changamoto hizo kwa undani na kutoa suluhisho ili kuweza kudhibiti baadhi ya wafanyabiashara kuingiza au kuuza ngozi kwa njia ya magendo.

Kuhusiana na hali ya soko la bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya ndani, anasema tayari wananchi wamehamasika kununua bidhaa zinazozalishwa nchini tofauti na kipindi cha nyuma, ambapo bidhaa za nje ndio zilikuwa zinapewa kipaumbele.

Anasema kwa sasa ubunifu umekuwa ni mkubwa jambo ambalo limechangia bidhaa za ndani kuaminiwa, na anatolea mfano wa viatu vya ngozi wanavyozalisha.

"Tunatengeneza viatu vya majeshi, kwa sasa hawaagizi tena nje ya nchi hii ni fursa mpya katika kukuza soko la ndani na kukuza sekta ya ngozi nchini kwa ujumla wake na hali inaelekea kuwa nzuri," anabainisha Woisso.

Pia anasema kuwa kiwanda cha WOP katika kuunga mkono jitihada za Serikali kuelekea uchumi wa viwanda wamejidhatiti kutengeneza bidhaa zenye ubora wa kimataifa ili kukuza soko la bidhaa za ngozi ndani na nje ya nchi.

## KUMBUKUMBU

**30/03/2011**



KANISIA SOTIKA KOMBA

**Ni miaka 11 toka ulipoitwa na Mwenyezi Mungu katika makao ya milele. Sisi tunaona ni kama siku 11 zimepita.**

**Tunaendelea kuona pengo lako kwenye maisha yetu.**

**Unakumbukwa sana na Mume wako Mzee Kayombo, watoto wako Betilda, Bosko, Cresensia, Joyce, Marietha na Julius, Wakwe zako, Wajukuu, Vitukuu, Kaka zako, Ndugu, Jamaa na marafiki.**

**Raha ya milele Umpe ee bwana na Mwanga wa milele umuangazi, Astarehe kwa amani.**

**AMINA**

## KUPOTEA KWA CHETI CHA SHULE



Mimi **PRINCE JOHN CHASAMA** wa Dar es Salaam natangaza kupotelewa kwa cheti changu cha shule **Index Namba S1022/0343 (Ordinary Certificate)** kilichotolewa na Baraza la Taifa la Mtihani mwaka 2015.

Kwa yeyote atakayekiona au kukiokota anaombwa kukiwasilishe katika Kituo chochote cha Polisi kilicho karibu. Taarifa imetolewa Polisi kwa Namba **DAR/CEN/RB/46945/2022 au piga simu +255786232789.**

Scanned with CamScanner

... wanatakiwa kutumia fursa hiyo ili wapate kuwa wakarimani ndani

Kunenge alisema mkoa una viwanda 1,453 vikiwamo vikubwa 87.

NIPASHE UK 5.

# Wafugaji wasimamisha kilimo Kwala

**Na Julieth Mkreri,** KIBAHA

BAADHI ya wakazi wa Kijiji cha Kwala Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha mkoani Pwani wameiomba serikali kusimamia suala la wafugaji kuhama katika kijiji hicho ili waendelee na shughuli za kilimo.

Wakizungumza na Nipashe, walisema wako hatarini kukumbwa na njaa kwa kuwa msimu huu wa kilimo hawajajishughulisha kwa kuhofia mazao yao kuharibiwa na mifugo.

Denis Makusanya alisema wamekuwa wakilima mazao, lakini baadhi ya wafugaji wanalisha mifugo yao kwenye mashamba ya wakulima bila hofu.

"Huku kwetu mihogo ndio tulikuwa tunategemea sana, lakini kwa sasa hakuna tena, mifugo imeharibu imekula mazao yetu yote shambani hata mbegu ya mihogo hatuna tena," alisema Denis.

Alieleza kuwa yupo mfugaji maarufu (anamtaja) alishaelezwa na viongozi wa serikali aondoke aende sehemu ya wafugaji, lakini hadi sasa hajatekeleza agizo hilo, na kwamba wapo wafugaji wengine wameshindwa kuondoka kwa sababu yake.

"Wapo watu wametoka mjini na kununua mashamba huku kwa ajili ya kilimo, lakini wamesimama kuendelea na shughuli zao kutokana na hawa wafugaji, huyu (mfugaji huyo maarufu) akiondolewa na wengine wataondoka wengi wako nyuma yake wanamsikiliza," alisema.

Frank Willson aliliambia Nipashe kuwa wamekuwa wakilalamikia suala hilo kwa viongozi kuanzia ngazi ya kitongoji hadi mkoa, lakini hadi sasa kero yao haijapatiwa ufumbuzi.

Kwa mujibu wa Frank, amesimamisha shughuli za kilimo tangu mwaka jana, baada ya kupata hasara mara kwa mara anapolima, badala yake ameamua kujikita katika uuzaji wa mkaa ili aweze kuendesha maisha.

Naye Ibrahim Lubeta, mjumbe katika kitongoji cha Mahundi, alieleza kuwa mbali na mazao kuharibiwa, wafugaji hao wamekuwa wakiwapiga wakulima.

"Wanaingiza mifugo yao shambani ukiwaambia waiondoe wanasema watachungia wapi, ukijaribu kuitoa isiendelee kuharibu mazao wanakupiga na kukuumiza... ukilalamika kwa uongozi wa juu hakuna utatuzi unaofanyika kwa wakati," alisema.

Hata hivyo aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhandis Evarist Ndikilo, aliwahi kufika na kusikiliza malalamiko ya wananchi hao ambapo alitoa maagizo kwa viongozi wa Wilaya na Tarafa ya Ruvu kuhakikisha wafugaji wanaondoka na kuhamia katika maeneo yao, agizo ambalo hata hivyo halijatekelezeka hadi sasa.

Pia alizuia wafugaji kulisha mifugo yao katika bonde la Mto Ruvu ambapo wakulima wengi wanalitumia kwa kilimo cha umwagiliaji agizo ambalo utekelezaji wake bado haujafanyika.

Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Sara Msafiri, alipoulizwa na Nipashe kuhusiana na malalamiko ya wananchi, hao alisema atashughulikia suala hilo.

Idadi kubwa ya wakazi wa Kijiji cha Kwala inaelezwa kuwa ni wakulima, huku wengine wakitoka katika mikoa mingine kuhamia katika kijiji hicho kwa ajili ya kilimo, lakini wamekwama kutokana na kubughudhiwa na wafugaji.

Scanned with CamScanner

Na Kija Elias

IDADI ya mifugo nchini inakadiriwa kuongezeka mwaka 2020/2021 ikilinganishwa na 2019/2020 ambapo idadi ya ng'ombe iliongezeka kutoka milioni 33.4 hadi milioni 33.9, mbuzi kutoka milioni 21.29 hadi milioni 24.5 na kondoo kutoka milioni 5.65 hadi milioni 8.5.

Kwa mujibu wa sekta ya mifugo mwaka 2020 ilikua kwa asilimia 5.0 na hivyo kuchangia asilimia 7.1 katika pato la Taifa ikilinganishwa na mwaka 2019, ambapo ilikua kwa asilimia 5 hatua iliyochangia asilimia 7.4 kwenye pato la Taifa mwaka huo.

Januari 3, 2022, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilizindua uhamasishaji na mafunzo kuhusu uvalishaji wa hereni za kielektroniki kwa mifugo ili kusaidia kupunguza migogoro na wizi wa mifugo hususan maeneo ya mipakani mwa Tanzania na nchi zingine ili kulinda maeneo ya malisho.

Akizungumza wakati wa uhamasishaji na mafunzo kwa wadau wa mifugo mkoani Kagera ikiwemo ngazi ya mkoa na wilaya zake, Dk. Auditas Sarimbo kutoka Idara ya Huduma za Mifugo, anasema mpango huo utasaidia mikoa iliyopo mipakani kudhibiti mifugo kutoka nchi jirani kuingia nchini. Na kwamba uingiaji wa mifugo kwa wingi umekuwa ukiharibu mazingira kutokana na wingi wa mifugo inayoingizwa bila utaratibu.

Dk. Sarimbo anafafanua kuwa lengo la kuweka hereni za kielektroniki kwa mifugo ni mfugaji kutambua mifugo yake, na Serikali kuweze kujua mifugo iliyopo, na hivyo kupunguza wizi na migongano maeneo ya mipakani, ambapo kuna mwingiliano wa mifugo pamoja na kudhibiti mifugo dhidi ya magonjwa kwa kufuatilia taarifa za mifugo hiyo.

Katika kuitikia agizo la Wizara ya Mifugo na Uvuvi la kutaka mikoa na wilaya zote nchini kuhakikisha mifugo yote inawekewa alama kwa ajili ya kuitambua ifikapo Machi 31, 2022, Serikali wilayani Mwanga imezindua mpango wa uvalishaji wa hereni za kieletroniki kwa mifugo yote iliyopo wilayani humo.

Akizindua mpango wa uvalishaji wa hereni za kielektroniki tukio lililofanyika katika kijiji cha Kwakahindi, kata ya Kigonigoni, Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, Abdallah Mwaipaya anasema wilaya hiyo inakabiliwa na changamoto ya makundi makubwa ya mifugo ambayo yamekuwa yakiingia na kusababisha uharibifu wa mazingira kutokana na mifugo inayoingizwa bila kufuata utaratibu.

Anasema Wilaya ya Mwanga imeathiriwa, na kwamba wilaya hiyo imekuwa tena maeneo ya kukusanya mifugo ambayo inakuja kutoka maeneo jirani kwa lengo la kutafuta malisho, na hivyo akawataka wafugaji wote waliloingiza mifugo yao bila kufuata utaratibu kwa ajili ya kutafuta malisho kuondoka haraka.



Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, Abdallah Mwaipaya akivisha ng'ombe hereni ikiwa ni ishara ya uzinduzi wa uvalishaji mifugo hereni za kielektroniki.

# Faida utambuzi wa mifugo kupitia hereni za kielektroniki

Alimwomba Ofisa Mifugo na Uvuvi wa Wilaya ya Mwanga, Emil Mkemwa kuwaandikia barua maofisa mifugo wa vijiji na kata kuacha tabia ya kutoa vibali kwa ajili ya kuruhusu mifugo kutoka maeneo jirani kuingia ndani ya wilaya hiyo kwa ajili ya kutafuta malisho.

"Lengo la kuweka hereni za kielektroniki kwenye mifugo ni mfugaji kutambua mifugo yake na Serikali kujua mifugo iliyopo hatua ambayo itasaidia kupunguza wizi na migongano inayohusisha mifugo maeneo ya mipakani, ambapo kuna mwingiliano wa mifugo pamoja na kudhibiti mifugo dhidi ya magonjwa kwa kufuatilia taarifa za mifugo hiyo," anasema Mwaipaya.

Anasema kwa sasa katika ngazi za kimataifa wafanyabiashara wanataka kufuata mifugo ya aina fulani, ambapo utambuzi wa mifugo umewekewa alama kuanzia ngazi ya Taifa na kijiji mfugo ulipo pamoja na jina la mmiliki wake.

"Serikali inataka kuwa na rekodi za mifugo yote, na hii ni takwa la kibiashara, mpango huu utasaidia Serikali na wafugaji kujua mifugo inatoka wilaya gani na nani anamiliki, pia itasaidia kuimarisha masoko ya mazao ya mifugo ndani na nje ya nchi ikiwa ni pamoja na kusaidia kudhibiti migogoro ya wakulima na wafugaji," anasema.

Anafafanua kuwa mpango wa uwekaji hereni za kielektroniki kwa mifugo upo kwa mujibu wa Sheria, ambayo inaelekeza mifugo yote nchini kusajiliwa, na mpango huu haujaletwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga, Mwajuma Nasombe anasema mpango wa uwekaji hereni za kieletroniki kwa mifugo una faida nyingi zikiwemo za wafugaji kupata mikopo benki pamoja na kuzuia wizi wa mifugo.

Aidha, anawahamasisha wafugaji wilayani humo kushiriki vyema katika mpango huo na kuachana na uwekaji wa alama kwa njia ya moto kwani zimekuwa zikisababisha mifugo kukosa soko katika baadhi ya nchi kwa kuwa ngozi za mifugo zinakuwa zimeharibiwa.

Nasombe anawashauri wafugaji kuhakikisha wanashiriki vyema katika mpango huo ili mifugo yao itambuliwe rasmi na kuwa rahisi kwa Serikali kupanga mipango ya upatikanaji wa huduma za mifugo.

Awali, akisoma taarifa fupi ya uwekaji wa hereni za kielektroniki kwa mifugo wilayani humo, Ofisa Mifugo wa wilaya hiyo, Emil Mkemwa anasema mpango uwekaji hereni za kielektroniki kwa mifugo una faida nyingi zikiwemo za ufuatiliaji.

Aidha, anataja faida nyingine kuwa ni kuweza kupata takwimu sahihi ya mifugo, kukabiliana na magonjwa ya mlipuko, kurahisisha biashara ya mifugo ndani na nje ya nchi pamoja na udhibiti wa wizi wa mifugo.

Anasema Wilaya ya Mwanga uwekaji hereni ulianza Februari 14, mwaka huu, baada ya kikao cha uhamasishaji kilichofanyika kata ya Mgagao na kuwakutanisha wafugaji wote.

"Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga inatarajia kuweka hereni zaidi ya ng'ombe 134,799, mbuzi 159,199, kondoo 80,699 na punda 1,657. hadi sasa jumla ya mifugo 7,879 zikiwemo ng'ombe 3,869, mbuzi na kondoo 4,010, zimeshavalishwa hereni za kielektroniki kwenye kata ya Toloha, Mgagao na Kigonigoni," anasema.

Baadhi ya wakazi wa kijiji cha Kwakahindi, Daniel Tingide na Isaya Moses waliwahamasisha wafugaji wenzao kushiriki vyema katika mchakato huo, na kuacha kuweka alama za moto kwani alama hizo zimekuwa zikisababisha mifugo kukosa soko.

Katibu wa Chama cha Wafugaji Wilaya ya Mwanga, Peter Molell anasema changamoto iliyosababisha uvalishaji mifugo hereni kusuasua ni baadhi ya wafugaji kuhamisha mifugo yao kwa ajili ya kutafuta malisho kutokana na ukame uliotokea mwaka jana.

Utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo kwa hereni za kielektroniki ambao unafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Mwaka 2011, unatekelezwa kwa mfugaji kulipia gharama ya Sh. 1,750 kwa ng'ombe na punda, na Sh. 1,000 kwa mbuzi na kondoo.

*Baadhi ya wakazi wa kijiji cha Kwakahindi, Daniel Tingide na Isaya Moses waliwahamasisha wafugaji wenzao kushiriki vyema katika mchakato huo, na kuacha kuweka alama za moto kwani alama hizo zimekuwa zikisababisha mifugo kukosa soko.*

Scanned with CamScanner